

## **AFYA KINGA**

### **UTANGULIZI**

Wilaya ya Ngara ni miongoni mwa Wilaya nane (8) zinazoundwa na Mkoa wa Kagera. Wilaya iko Kaskazini Magharibi mwa Tanzania na inapatikana na nchi ya Rwanda kwa upande wa Kaskazini magharibi na Burundi kwa upande wa Kusini Magharibi. Aidha, kwa upande Mashariki Wilaya inapakana na Wilaya ya Biharamulo, upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Karagwe, na upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Kakonko Mkoa wa Kigoma. Wilaya ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 3,744 ambazo ni sawa na hekta 374,400. Wilaya hii imegawanyika katika Tarafa 4 ambazo ni Nyamiaga, Kanazi, Rulenge na Murusagamba. Tarafa hizo zina jumla ya Kata 22, Vijiji 75, na Vitongoji 394, Mamlaka za mji mdogo 2 ambazo ni Ngara Mjini na Rulenge. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 wilaya ina jumla ya Kaya 63,293, zenye watu 320,056 ambao kati ya hao 152,443 ni wanaume na 167,615 ni wanawake. Aidha, wanawake ni asilimia 52 na wanaume asilimia 48. Ongezeko la watu katika sensa ya mwaka 2002 na sensa ya mwaka 2012 ni asilimia 2.7.

Afya kinga katika Halmashauri ya wilaya ipo chini ya Afisa Afya Wilaya (DHO), ambae ni msimamizi na mshauri mkuu wa shughuli zote za Afya Kinga katika Wilaya. Wilaya yetu inatekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira katik avijiji vyote vya wilaya, ambayo inayo onyesha kaya wenye vyoo bora ni 59%, wenye vyoo hafifu ni 39.9%, wasio na vyoo kabisa 1.1% na wanaonawa mikono ni 14% ya 57934 ambazo kaya zilizotembelewa kati ya kaya 71803. Wilaya ya Ngara ina jumla ya vituo 53 vinavyotoa huduma za chanjo kati ya vituo vyote 61.

Afya kinga katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ina jumla ya vitengo 12 kama inavyo onyeshwa katika jeduari namaba 1:-  
Jadwari Na.1

### **MALENGO**

- Kuimarisha ubora na ufanisi katika utoaji wa huduma za kinga ili kuzuia maradhi na ulemavu, kwa kuboresha usafi wa mazingira ulio endelevu na hivyo kupunguza vifo na gharama za kutibu magonjwa.
- Kujenga ushirikiano kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kijamii na jamii katika kutoa huduma za afya.
- Kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.
- Kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yale ya mlipuko kwa Kuboresha ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza na mlipuko kwa kuanzisha daftari la tetesi

### **MAFANIKIO**

- Kaya zipatazo 34,181(59%) zimeweza kujenga vyoo bora na kuvitumia, kwa kupitia Viongozi wa vijiji 66 vya wilaya ya Ngara wameweza kuhamasishwa juu ya kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira hivyo imewezesha Kutokuwepo magonjwa ya mripuko ndani ya wilaya yatokanayo na uchafuzi wa mazingira.
- Uwepo na ushirikishwaji wa wadau na kusaidia kutoa huduma za afya wilayani Ngara.

- Kudhibiti vyakula vyenye athari kwa watumiaji kwa Kutoa elimu kwa wadau husika na Kuedelea kusajili majengo ya vyakula yenye sifa.
- Kupunguza vifo vya watoto wadogo chini ya miaka mitano kwa kupitia maendeleo ya huduma za Afya kwa jamii na utoaji wa chanjo
- Kudhibiti magonjwa mengine ya maambukizi kupitia ufuatiliaji wa magonjwa na utumaji wa taarifa kielektroniki kwa wakati kwa asilimia 98. [disease surveillance na eIDSR]

## **CHANGAMOTO**

- Bajeti ya Usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ni 2%, hivyo inapelekea kukwamisha baadhi ya shuhuli za utendaji kwa ajili ya kuzuia magonjwa yatokanayo na Mazingira hatarishi.
- Kuwepo na watumishi wachache wa Afya mazingira ambao ni 8, na mahitaji ni 33, hivyo kuna upungufu wa 25.
- Vikao vya kila robo na wadau wanaotoa huduma za Afya kushindwa kufanyika kutokana kutokuwepo bajeti maalum.
- Uanzishwaji holela wa biashara ya vyakula kwa maeneo yasiyo rasmi
- Kutokuwepo kwa vyombo vya usafiri vya kutosha kwa watumishi kama pikipiki na vitendea kazi kama komputa.
- Baadhi ya frige ni mbovu na hakuna spea zake.
- Kutokuwepo kwa vikinga mwili PPE hasa hasa za Ugonjwa wa Ebola.

## **MIKAKATI/ UTATUZI**

- ❖ Kuongeza bajeti ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri ya Wilaya angalau 30% ili kuwezesha shughuli za kuzuia magonjwa yatokanayo na mazingira.
- ❖ Halmashauri ya Wilaya kuwaomba TAMISEMI kuwaengezea watumishi wa Afya Mazingira angalau 10, ili kuweza kufikia malengo ya uzibiti maradhi katika Wilaya.
- ❖ Kuendelea kutumia sheria za udhibiti wa vyakula ,dawa na vipodozi
- ❖ Halmashauri ya Wilaya kuongeza vyombo vya usafiri kama vile pikipiki na vitendea kazi kama vile komputa ili kuzidisha ufanisi wa kazi.
- ❖ Tunaomba wizara ifanye mchakato wa kutuongezea majokofu kwani vituo vimeongezeka kutoka 48 mwaka 2014 hadi 53 mwaka 2018
- ❖ Kila kituo cha Afya kuhakikisha kununua kwa vikinga mwili (PPE) kwa kutumia hela za RBF, hasa hasa za ugonjwa wa Ebola angalau angalau moja moja.